Hali kadhalika mfumo huu umetusaidia kufahamu miamala mbalimbali ya kifedha inayofanyika kwa njia ya mitandao; ambamo tumesikia kwamba mwaka jana miamala yenye thamani ya shilingi trilioni 139.2; wastani wa trilioni 11.6 kwa mwezi

ilifanyika. Hii imeiwezesha Benki Kuu ambayo ndiyo msimamizi mkuu wa masuala ya fedha nchini – na nimeshukuru kumuona Naibu Gavana yupo hapa – kufahamu idadi ya miamala ya fedha inayofanyika kwa njia ya kimtandao.

Siku za nyuma miamala ya fedha ilikuwa haijulikani.

Hali kadhalika mfumo huu umeiwezesha Mamlaka yetu ya Mapato kukusanya mapato yake stahiki kutoka kwa watoa huduma, tofauti na zamani ambapo ilitegemea zaidi taarifa kutoka kwa watoa huduma.

Mradi huu umetekelezwa kwa ubia kati ya serikali na sekta binafsi, kwa utaratibu wa jenga, endesha na hamisha umilki, yaani *build, operate and transfer*. Kwa mujibu wa mkataba, mkandarasi akitakiwa kujenga mfumo huu, kisha auendeshe mwenyewe, baada ya miaka kadhaa aukabidhi serikali; na ndio maana leo amekabidhi serikali na unabaki kuwa mali ya serikali kwa asilimia mia moja. Hongereni sana.

Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza wale wote waliobuni wazo la kutekeleza mradi huu. Aidha nampongeza mhandisi kwa kutekeleza mradi huu kwa mujibu wa mkataba.

Nafahamu kuwa kuna wakati tulivutana, kama nilivyoeleza, na tulivutana kidogo kidogo ingawaje kwa kuzingatia maslahi mapana ya serikali. Nafurahi hatimaye tulikubaliana na mkataba umekamilika; na hiki ni kielelezo kuwa nchi yetu iko tayari kushirikiana na sekta binafsi katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Tumekuja hapa kushuhudia makabidhiano ya mfumo na naomba mniruhusu niseme mambo machache ya mwisho.

Kwanza napenda kuwapongeza TCRA kwa kupata mfumo huu wa kisasa wa kusimamia mawasiliano ya simu. Ni imani yangu kuwa mfumo huu utawezesha kutekeleza majukumu yenu ipasavyo. Wito wangu kwenu: msiachie tu kuupokea mfumo huu; hakikisheni mnajijengea uwezo, sio tu katika kusimamia na kuendesha mfumo huu lakini pia katika kuuboresha, kuupanua mfumo wenyewe na kuulinda.

Yaliyotokea kwenye EFD nisingependa yatokee kwenu. Kwenye EFD mnafahamu kilichotokea na Kamishna wa TRA anafahamu kilichotokea. Walikuwa na mfumo lakini hawakuweza kuusimamia wao. *Server* haikuwa Tanzania.

Nilipofika hapa nikauliza: '*server* iko hapa?' Wakanionyesha *server* iko hapa hapa. Nikasema hapo ndipo sawasawa. Hongereni sana TCRA. Mmekuwa na akili.

Bila hivyo *server*, ingekuwa huko, *wanaoperate*

wanavyotaka, ninyi mnabaki na picha. Ndio ujanja wa kimataifa wa leo. EFD walichezewa hivyo hivyo. *Server* ilikuwa kwingine, nchi nyingine; wao wana EFD hapa. Lakini walijitahidi. Nampongeza Kamisha Mkuu wa TRA; wamebadilisha mfumo huo wa EFD umekuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha yenyewe. Hongereni sana.

Saa nyingine tunajifunza kwa makosa lakini sio vizuri kurudia makosa kila mara.

Zaidi ya hapo umuhimu wa kujenga uwezo unakuja kwa sababu sekta ya mawasiliano inabadilika na kukua kwa kasi kubwa. Nimeeleza kuhusu biashara ya kimtandao, e-commerce, masuala ya usafiri, Uber na Taxify, upigaji simu kwa njia ya *whatsapp, skype, immo* na kadhalika. Sina uhakika kama mfumo wenu huu una uwezo wa kufuatilia takwimu kwenye maeneo hayo.

Hivyo basi natoa rai kwa TCRA ikishirikiana na mamlaka nyingine nchini ikiwemo Wakala wa Serikali Mtandao kujiimarisha kiutaalamu ili kuweza kushughulikia masuala hayo.

Pili, tumeona hapa kuwa moja ya manufaa yaliyoletwa na ukuaji wa sekta ya mawasiliano ni kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Hivyo basi napenda kutumia fursa hii kurudia agizo langu kwa taasisi zote za serikali zenye kukusanya mapato kuhakikisha kwamba zinatengeneza mfumo wa kielektroniki katika kukusanya mapato.

Ninaiagiza pia Wizara ya Fedha – na bahati nzuri pia Waziri yuko hapa – kuhakikisha taasisi zote za serikali zinaunganishwa na mfumo mkuu wa ukusanyaji wa fedha za umma, government *e-payment system* na *gateway* ya GePG.

Nimeambiwa kuwa kati ya taasisi 667 zenye kustahili mpaka sasa zimeunganishwa taasisi 339 tu; nyingine bado.

Sasa Waziri yuko hapa; nitashangaa sana hizi taasisi ambazo ni mali ya serikali, ni mali ya wananchi ziendelee kukaa tu bila kuunganishwa kwenye mfumo huu.

Nitawashangaa mawaziri walioko kwenye wizara hizo wanazosimamia hizo taasisi na makatibu wakuu wa taasisi hizo. Kama wataendelea kutoziunganisha maana yake wana lengo la kufanya biashara gizani, iliyozungumzwa na Mheshimiwa Spika hapa; na mimi nisingependa kuona taasisi ninazoziongoza bado zinaendelea na biashara ya gizani. Tunataka tuwe na tochi; tujue wanachokifanya huko.

Kwa hiyo ni matumaini yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha utawaandikia barua, na hasa taasisi hizo zote, na nakala umpe Waziri Mkuu na unipe na

mimi ili niendelee kuchungulia pole pole.

Hakikisheni mnaziunganisha taasisi zote zilizobaki. Mfumo wa GePG unahusika na ukusanyaji wa fedha kwa njia ya kielektroniki na una faida nyingi. Pamoja na kuongeza mapato kama tulivyoona hapo kwa TTMS, unapunguza urasimu katika ukusanyaji, gharama za ufuatiliaji pamoja na kupunguza vitendo vya rushwa.

Nitatoa mfano mmoja. Kabla ya kujiunga na GePG, shirika la umeme, TANESCO lilikuwa kila mwaka likilipia zaidi ya shilingi bilioni 38 kwa wakala wa kuuza umeme. Baada ya kujiunga na mfumo wa GePG, sasa hawalipi hata senti moja; wanalipa ziro. Kwa hiyo wameokoa bilioni 38 kwa mwaka.

Hivyo basi narudia tena kutoa wito kwa taasisi za umma kukusanya mapato kwa njia ya kielektroniki na kujiunga kwenye GePG. Aidha tumieni tekinolojia ya mawasiliano katika kupata na kutunza taarifa zenu.

Tatu napenda kutoa wito kwa Watanzania kutumia vizuri sekta hii ya mawasiliano.

Sekta hii kama ilivyo mtu ananunua panga, au ananunua jembe au hata kisu au bunduki. Vifaa hivi vimetengenezwa ili kumuwezesha binadamu kuendesha shughuli zake na kujiletea maendeleo lakini ukivitumia vibaya vina uwezo wa kukuletea madhara makubwa; na sekta ya mawasiliano ni hivyo hivyo.

Licha ya manufaa yake mengi, sekta hii kama nilivyosema inaweza kuleta athari kubwa. Baadhi ya athari ni kuongezeka vitendo vya uhalifu duniani. Imechangia mmomonyoko wa maadili katika jamii. Sehemu nyingine mtu anajipiga picha yuko utupu halafu ana *post*.

Lakini pia imesababisha sehemu nyingine vurugu katika nchi. Mtu anaandika, anahamasisha vitendo vyovyote vya ajabu. Hivyo ninawasihi Watanzania wenzangu, tuepuke vitendo ambavyo vitaifanya sekta ya mawasiliano kuleta madhara kwenye nchi yetu.

Ni kama yule mtu aliyenunua panga kwa ajili ya kufyekea pori anajifyeka mwenyewe. Panga ni zuri kwa kufyekea, jembe ni zuri kwa ajili ya kulima na kupata mazao lakini ukilitumia kumkata mtu mwingine jembe hilo hilo linakuwa baya.

Nitoe rai kwa Mamlaka ya Mawasiliano: kuweni wakali dhidi ya watu wanaotumia vibaya huduma za mawasiliano. Msiwaonee huruma. Tumieni sheria katika kuhakikisha vitendo vya ovyo vinavyofanyika kupitia huduma ya mawasiliano vinakoma.

Katika hili nitoe pia wito kwa TCRA, kuharakisha

zoezi ya usajili wa laini za simu kwa njia ya ya biometria ili kudhibiti vitendo vya uhalifu.

Suala la nne na la mwisho, nafurahi Mkurugenzi Mkuu ameligusia kidogo: ni kwamba kama nilivyosema awali, nchi yetu ina vifaa vingi vinavyotumia mtandao – simu, kompyuta, *gadgets* na kadhalika na nafahamu kwa mujibu wa sheria na kanuni za kimataifa watengenezaji wa vifaa hivyo wana wajibu wa kutoa mchango pindi pale vifaa hivyo vinapofika ukomo wa kuvitumia; viweze kuharibiwa, kugeuzwa na kutumiwa kwa matumizi mengine.

Hivyo basi kwa kuwa kwa sasa tunao mfumo unaotuwezesha kutambua vifaa vyote vinavyotumia mtandao nchini ingefaa muanze kufuatilia kwenye kampuni zinazotengeneza vifaa hivyo ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria za kimataifa.

Napenda kuhitimisha kwa kurudia tena kushukuru kwa kunialika kuja kwenye shughuli hii. Aidha naipongeza Mamlaka ya Mawasiliano kwa kazi kubwa na nzuri mnayoifanya na nasema mnafanya kazi nzuri sana. TCRA fanyeni kazi. Msiogope. Mtangulizeni Mungu katika kazi zenu. Msiogope vitisho; chapeni kazi kwa niaba ya Watanzania. TCRA iko pale kwa niaba ya Watanzania wote katika kushughulikia masuala ya mawasiliano.

Mwisho kabisa, narudia tena kuwashukuru sana makandarasi kwa kutekeleza wajibu wao na niwaombe kunapotokea matatizo yoyote katika mitambo hii wasisite kuja kushirikiana na TCRA katika kufanya marekebisho; na niwaombe TCRA kuhakikisha mnaitunza mitambo hii. Naomba vyombo vya ulinzi na usalama vihakikishe vinashirikiana na TCRA katika kuhakikisha TTMS inalindwa kikamilifu.

La mwisho kabisa, napenda kuwashukusu sana viongozi wa dini, niwashukuru sana. Endeleeni kuliweka Taifa hili kwenye mikono ya Mungu. Hii ni vita kama ilivyo vita nyingine.

Vita ya uchumi inahitaji maombi. Bila maombi kazi hii haiwezi ikafanyika. Hao wanaokaa gizani, huwezi kujua iwapo mtu ana panga, ana kisu, ameshikilia nyoka mfukoni au ana kitu gani. Lakini huko gizani huwa wanatolewa kwa maombi.

Ndio maana nasisitiza ndugu zangu viongozi wa dini wote kwa umoja wenu: endeleeni kuliweka taifa hili katika maombi ili sisi pamoja na serikali na watendaji wengine wote tuendelee kusimamia misingi ya uadilifu na upendo wa kweli wa Mungu katika kulitumia taifa hili.

Mungu ubariki mfumo huu wa TTMS, Mungu ibariki Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Mungu ibariki Tanzania, Mungu wabariki wote waliohudhuria

Mkurugenzi Mkuu TCRA, Mhandisi James M.Kilaba akionyesha kitabu cha mwongozo wa mfumo wa TTMS baada ya kukipokea kutoka kwa Mkandarasi wa mradi huo. Kushoto ni Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Mamlaka, Bw. Johannes Karungura

Usimamizi wa kimkakati

Maelezo ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mh. Mhandisi Isack Kamwelwe (MB)

Mfumo huu wa usimamizi wa Mawasiliano ya simu (TTMS) ambao leo tunashuhudia kukabidhiwa rasmi kwa Serikali ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 ambayo imetuelekeza kuboresha mawasiliano na sekta nzima ya mawasiliano ili sekta hii ichangie katika kuboresha maisha ya mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla kiuchumi na kijamii.

Mfumo huu wa usimamizi wa mawasiliano ya simu ni mojawapo ya miundombinu muhimu katika kuongeza ufanisi wa usimamizi wa sheria na kanuni zinazosimamia sekta ya mawasiliano. Usimikaji wa mfumo wa TTMS ulifanyika kwa mujibu wa Kanuni za Mawasiliano ya Kielekroniki na Posta (TTMS) ya mwaka 2013 na ambazo zilihuishwa mwaka 2018 pamoja na makubaliano yaliyoingiwa kati ya Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano na Mkandarasi SGS na GVG (*SGS, GVG consortium)* yaliyoingiwa tarehe 1 Oktoba, 2013.

Lengo la usimikaji wa mfumo huu ni kuhakikisha kuwa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano yanakuwa na manufaa kwa nchi kwa kuchangia ipasavyo katika mapato ya Serikali na kukuza uchumi.

Tangu kuanzishwa kwake mwezi Oktoba 2013, mfumo huu umesaidia katika kusimamia miamala ya fedha inayofanyika kupitia mitandao ya makampuni ya simu hapa nchini, kuzuia matumizi ya vifaa vya mawasiliano ya simu visivyo na ubora katika mtandao wowote wa simu hapa nchini, kubaini mawasiliano ya simu za ulaghai; na kupatikana kwa takwimu za mapato yatokanayo na huduma za mawasiliano zinazotolewa na kampuni za simu hapa nchini. Takwimu zinaonyesha ongezeko la laini za simu kutoka 39,808,419 mwaka 2015 hadi kufikia laini za simu 42,961,449 mwaka 2018.

Kwa taarifa zilizopo tangu mfumo huu uanze kufanya kazi mwezi Oktoba 2013 hadi kufikia mwezi Disemba 2018 mfumo huu umewezesha Serikali kukusanya jumla shilingi za Kitanzania 93,665,645,344.55. Pia umeweza kutoa taarifa mbalimbali zinazohusiana na biashara ya huduma ya mawasiliano kwa mamlaka husika.

Kabla sijakukaribisha ili uzungumze na hadhira hii, niruhusu nizungumze kwa ufupi mafanikio ya Sekta ya Mawasiliano tangu kuingia kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 Ibara ya 47 (g), (i) na (j):

Ibara ya 47(g) inatuelekeza kuendelea kuweka mazingira bora ya ushindani kwenye sekta ya mawasiliano ili wananchi wengi waweze kumudu gharama za mawasiliano ya simu.

Serikali imeweka ukomo wa gharama za mwingiliano kwa huduma za mawasiliano (*inteconnection*) ambao unatakiwa uzingatiwe na watoa huduma wote wa mawasiliano kati ya mtandao mmoja na mwingine; ambapo gharama ya maunganisho ya mitandao imepungua kutoka shilingi 30.58 kwa dakika mwaka

2015 hadi kufikia 10.40 kwa dakika mwaka 2019 na itaendelea kupungua hadi shilingi 2.00 ifikapo mwaka 2022.

Ibara ya 47 (i) inatuelekeza kuwalinda watumiaji wa simu za mkononi dhidi ya dhuluma, wizi na uhalifu wa mitandao;

• Usimamizi wa Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 pamoja na Kanuni za Huduma za Ziada za mwaka 2015 umewezesha kwa kiasi kikubwa kudhibiti uhalifu wa mtandao, japokuwa mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia yanaleta changamoto katika kudhibiti.

• Kukamilika kwa mfumo wa usajili kwa kutumia alama za vidole katika kuhakiki taarifa za watumiaji wapya wa laini za simu umezinduliwa, na unategemewa utakapokamilika utasaidia kupunguza matukio ya kihalifu na kurahisisha ufuatiliaji unaofanywa na vyombo vya usalama pale inapotokea changamoto za kiusalama au za jinai;

• Elimu inaendelea kutolewa kwa wananchi kuhusu uhalifu katika mtandao na namna ya kuubaini, kuchukua tahadhari na kutoa malalamiko au taarifa kwa vyombo vinavyohusika.

Ibara ya 47(j) inatuelekeza kuongeza idadi ya watumiaji mitandao ya intaneti kutoka milioni tisa (9)mwaka 2015 hadi kufikia milioni 20 mwaka 2020.

Idadi ya watumiaji wa mitandao ya intaneti imeongezeka kutoka watumiaji 9,312,272 mwaka 2015 hadi kufikia watumiaji 22,995,109 mwezi Desemba, 2018, hivyo kuvuka lengo lililokusudiwa.

Kuwepo kwako hapa leo hii, kunathibitisha nia ya Serikali ya Awamu ya Tano na wewe binafsi kuwa sekta ya mawasiliano ni muhimu katika kuinua maendeleo ya uchumi wa Taifa letu kwani inawezesha kuongeza ufanisi katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

Nimalizie kwa kukushukuru tena kwa kuja kujumuika nasi katika tukio hili. Nawashukuru pia Bodi na Menejimenti ya TCRA kwa ushirikiano wenu katika kusimamia sekta ya mawasiliano nchini. Aidha naishukuru sana Kamati ya Katibu Mkuu Kiongozi ambayo imefanya kazi kubwa kuhakikisha maboresho ya mfumo wa TTMS yanafanyika kwa kuzingatia maelekezo uliyoyatoa.

Baada ya kusema hayo, nikuombe Mheshimiwa Rais ushuhudie kukabidhiwa rasmi Mfumo wa TTMS, ambapo TCRA itatoa Hati ya Kukamilika kwa Mradi na Mkandarasi atakabidhi kitabu cha mradi na mwisho nikuombe uongee na hadhira hii pamoja na wananchi wote wanaokusikiliza kupitia vyombo vya habari.

Idadi ya akaunti za pesa mtandao, 2018

Mtandao	Oktoba	Novemba	Desemba
M - Pesa	9,033,134	9,055,571	9,014,088
Tigo Pesa	7,416,770	7,545,235	7,586,240
Airtel Money	4,243,577	4,720,503	4,848,545
Halopesa	935,662	1,268,626	1,342,206
Ezy Pesa	331,248	344,501	546,353
T - PESA	33,655	33,781	30,394
Jumla	**21,994,046**	**22,968,217**	**23,367,826**

Nyenzo mpya ya uhakiki kodi

Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Mh. Dkt Philip Mpango

Mfumo huu wa usimamizi wa mawasiliano ya simu (TTMS) ambao leo tunashuhudia kukabidhiwa kwa Serikali ni mojawapo ya miundombinu muhimu katika kuchochea uchumi na maendeleo ya Taifa.

Naipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kuweka Mfumo ambao umewezesha kupatikana kwa chanzo kipya cha mapato yasiyo ya kodi kwa kila mwezi, ambapo hadi kufikia Disemba 2018 Serikali imepata jumla ya Shilingi za Kitanzania 93,665,645,344.55.

Aidha, mfumo wa TTMS umeisaidia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhakiki mapato kutoka kampuni za simu na hivyo kutekeleza jukumu lake kuu na la msingi la ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Utaratibu wa kulipia kodi duniani kwa sasa na ambao pia unatumiwa na TRA ni mfumo wa mlipa kodi kujikadiria mwenyewe kiasi cha kodi anachostahili kulipa (*self-assessment*), na kisha mlipa kodi kuwakilisha makadirio yake kwa mamlaka za usimamizi wa kodi katika utaratibu wa ritani zinazowalishwa kwa mujibu wa sheria.

Kampuni za simu kama walivyo walipa kodi wengine, huwasilisha kwa wakati ritani zao za makadirio ya kodi na ushuru yanayotakana na vyanzo vyao vya mapato.

Kabla ya kuanza kwa mfumo huu wa TTMS, TRA haikuweza kuhakiki kwa ufanisi ritani mbalimbali zilizokuwa zinawasilishwa na kampuni za simu kutokana na wingi na ugumu wa taarifa za utendaji wao kifedha. Mara zote, TRA ililazimika kuzipokea na kuzihakiki ritani hizi bila kuwa na nyenzo zenye ubora na uhakika kama mfumo wa TTMS.

Mfumo wa TTMS kama nyenzo mpya ya ukaguzi unaiwezesha TRA kuhakiki taarifa za kodi za kampuni za simu kwenye matamshi yao (*self-declaration*) ya kiasi halisi cha mauzo yatokanayo na huduma na bidhaa za mawasiliano kama vile data, sauti, na ujumbe mfupi na mauzo yatokanayo na tozo kwenye miamala ya fedha zinazosafirishwa kwa njia ya mtandao.

Hakika, mfumo huu wa TTMS umekuwa nyongeza ya nyenzo muhimu ya kiukaguzi kwa TRA katika kuhakikisha kodi stahiki inalipwa na tena kwa wakati, na huku ikiongeza utii (*compliance*) wa matakwa ya sheria kwa wateja.

Kupitia mfumo wa TTMS Benki Kuu (BOT) imepata nyenzo nyingine ya kuhakiki taarifa za miamala ya fedha kupitia mitandao ya simu.

Taarifa hizi zinatumika katika kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa fedha na kutekeleza sera za fedha na uchumi zinazosaidia Taifa kufikia lengo lake la kuwa nchi ya uchumi wa kati kufikia mwaka 2025.

Kipindi cha kuanzia Januari hadi Disemba 2018, miamala ya fedha kupitia simu za mikononi ilifikia

thamani ya shilingi 139.2 trilioni ambalo ni ongezeko la asilimia 35.2 ikilinganishwa na mwaka 2017 kutokana na kuenea kwa mawasiliano ya simu katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na upatikanaji wa huduma zinazolipiwa kwa kutumia simu za kiganjani.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na FinScope mwaka 2017, kufikia Disemba mwaka 2017, asilimia 72.3 ya Watanzania walikuwa na uwezo wa kutumia mifumo rasmi ya fedha.

Hili linaonesha mafanikio ya ushirikiano kati ya BOT na TCRA katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma za kifedha nchini.

Uwepo wa Sheria ya Mifumo ya Malipo na TTMS, vinachangia uimarishwaji wa matumizi ya mifumo rasmi ya fedha, hivyo kuchangia katika kuongeza pato la Taifa. Mfumo wa TTMS unasaidia katika udhibiti wa huduma za fedha kwa njia ya mitandao ya simu ambazo zimesaidia kusogeza utoaji wa huduma za kifedha vijijini. Vile vile utasaidia kuongeza uwazi katika tozo za huduma za fedha kwa njia ya mitandao ya simu.

Sheria ya Mifumo ya Malipo ya mwaka 2015 inatoa fursa sawa kwa wadau mbalimbali kushiriki katika kutoa huduma za malipo maeneo yote nchini. Usimamizi thabiti wa Kanuni zake unasaidia kuendelea kwa usambazaji wa mifumo ya malipo katika maeneo mbalimbali hata yale yasiyo na huduma za kibenki.

Sheria hii inasaidia utekelezaji wa mkakati mahsusi wa kuwezesha ujumuishwaji wa Taifa katika masuala ya fedha wa mwaka 2018-2022 (*National Financial Inclusion Framework, 2018*). Huu mkakati umeainisha namna Serikali na vyombo vyake vitakavyoweza kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazozuia huduma za kifedha kufikia maeneo mbalimbali ya nchi hususan vijijini.

Wizara ya Fedha na Mipango, pamoja na Taasisi zake za BOT na TRA tutaendelea kuutumia Mfumo huu katika utendaji wetu wa kila siku kwa manufaa

Baadhi ya watumishi wa TCRA na wadau wengine katika sherehe ya makabidhiano ya mfumo wa TTMS

Malengo saba ya ufanisi

Maelezo ya Mkurugenzi Mkuu
TCRA, Mhandisi James M. Kilaba

Chimbuko la usimikaji wa Mfumo huu wa kuratibu na kusimamia mawasiliano ya simu (Tele-Traffic Management System –TTMS) lilikuwa ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali yenyewe baada ya kushuhudia jinsi gharama kwa dakika kwa simu za kimataifa zilizokuwa zinaingia kwenye nchi yetu zilivyokuwa zinashuka kila leo. Hali hii ilikuwa inapunguza sana mapato kwa watoa huduma za mawasiliano nchini, ilikuwa inapunguza kodi kwa Serikali; na mchango katika uchumi wa nchi kwa ujumla ulipungua pia.

Kutokana na hali hiyo kulionekana mahitaji ya kuwepo mfumo wa kudhibiti changamoto hiyo.

Katika kutekeleza mahitaji ya uwepo wa mfumo huo, TCRA kwa kushirikiana na wadau wengine walisimamia taratibu za manunuzi ili kumpata mkandarasi ambaye alitokana na muungano, yaani *consortium* wa makampuni mawili ambayo ni Societe Generale de Surveillance S.A (SGS) na Global Voice Group S.A (GVG).

Mkataba kwa ajili ya usimikaji wa mfumo huo wa TTMS ulisainiwa tarehe 22 Machi, 2013 kati ya TCRA na muungano (*consortium*) wa SGS/GVG

kwa lengo la kutekeleza mradi huu. Hata hivyo Mkataba huo ulifanyiwa mapitio mara mbili na kuwekewa nyongeza (*addenda*) mbili zenye lengo la kuweka mkazo zaidi kwenye maeneo muhimu ya kiufundi na utekelezaji.

Utaratibu wa usimikaji wa mfumo huu wa TTMS ulikuwa wa kujenga, kuendesha na kuhamisha umiliki (*build, operate and transfer*) na ulianza kufanya kazi rasmi tarehe 1 Oktoba 2013.

Mkataba huo wa TTMS ulikuwa wa miaka mitano (yaani miezi sitini) na umemaliza muda wake tarehe 30 Septemba, 2018.

Kwa hatua hiyo, leo tunakabidhiwa rasmi Mfumo huo wa TTMS.

Serikali kupitia TCRA iliweka Mfumo huu ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa Sheria na Kanuni zinazosimamia sekta ya mawasiliano ikiwa ni pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya kasi yanayotokea katika sekta ya mawasiliano duniani kote.

Mfumo huu baada ya kukamilika, umewezesha kubaini takwimu mbalimbali za mawasiliano yanayopita katika mitandao ya mawasiliano.

Mfumo huu unaundwa na moduli kuu (*modules*) ambazo pamoja na mambo mengine umewezesha TCRA kwa yafuatayo: -

1. Kupata takwimu za mawasiliano ya simu yanayofanyika ndani na nje ya nchi (local and international traffic);

2. Kuhakiki mapato yote ya watoa huduma za Mawasiliano nchini;

3. Kupata takwimu zinazohusiana na matumizi ya huduma za mawasiliano (simu za sauti, matumizi ya data, na ujumbe mfupi).

4. Kugundua mawasiliano ya simu za ulaghai (*fraudulent traffic*);

5. Kutambua takwimu za ada za miamala ya fedha mtandaoni (*mobile money transaction*);

6. Kusimamia kwa ufanisi ubora wa huduma za mawasiliano (q*uality of service)* na hivyo kuboresha viwango vya huduma hizo;

7. Kutambua taarifa za laini ya simu (*SIM card profile)* na namba tambulishi za kifaa cha mawasiliano;

8. Kubaini na kufungia simu zenye namba

tambulishi zilizonakiliwa (*duplicate IMEIs*);

9. Kuwasilisha kwa Serikali mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu za kimataifa zinazoingia na kuishia hapa nchini.

Kuanzia Oktoba 2013 mfumo ulipoanza kufanya kazi mpaka Septemba 2018, Serikali imeweza kupata chanzo kipya cha mapato yanayotokana na mawasiliano ya simu za kimataifa zinazoingia na kuishia hapa nchini; na jumla ya shilingi za Kitanzania 93,665,645,344 ziliwasilishwa Serikalini.

Kabla ya kuwepo kwa TTMS, watoa huduma wetu walikuwa wakilipwa na makampuni ya nje senti nane hadi tisa za dola ya Kimarekani kwa kila dakika ya maongezi kwa simu zinazoingia na kuishia hapa nchini.

Baada ya kusimika TTMS sasa wanapata senti 13; ikiwa ongezeko la senti nne hadi tano, hivyo kuongezeka pia kwa mapato yao na kodi kwa Serikali yetu.

Kabla ya Mfumo huu wa TTMS, simu za kimataifa zilizokuwa zinaingia hapa nchini kwa njia za ulaghai (*illegal routes*) zilikuwa asilimia sitini na tano (65%) ya simu zote za kimataifa zilizokuwa zinaingia nchini, zilizofanyiwa majaribio. Hii ina maana mapato ya watoa huduma na kodi za Serikali zilikuwa zinapotea kwa asilimia hiyo pia.

Mfumo huu umeiwezesha TCRA kwa kushirikiana na vyombo vingine kuwabaini watu wenye mifumo ya ulaghai ya kuingiza mawasiliano ya simu kutoka nchi za nje, ambapo wahusika wa matukio hayo wamekuwa wakifikishwa kwenye vyombo vya sheria kwa ajili ya hatua stahiki.

Kwa sasa kiwango cha simu za kimataifa zinazoingia hapa nchini kwa njia za ulaghai (illegal routes) ni chini ya asilimia kumi (10%) ya simu zote za kimataifa zinazoingia nchini zilizofanyiwa majaribio.

Zoezi la kubaini simu hizo za ulaghai zinazoingia hapa nchini ni endelevu, kwa kuwa wahalifu hubuni njia mbalimbali kila wakati za namna ya kuingiza mawasiliano kwa njia za ulaghai ili wajipatie mapato hayo haramu.

Mfumo huu umeongeza usalama mtandaoni kwa watumiaji wa vifaa vya mawasiliano vyenye namba tambulishi (IMEI) halisi.

Kwa mfano mfumo huu umewezesha kubaini, kuchunguza na kuzifungia simu 1,675,277 zilizokuwa zikitumika kwenye mitandao mbalimbali zikiwa na IMEI bandia au zilizochakachuliwa. Idadi hii inajumuisha simu zilizoripotiwa kutokufikia viwango vinavyotakiwa, simu z i l i z o r i p o t i w a

kuibiwa pamoja na simu zilizoripotiwa kupotea.

Mfumo huu pia unawezesha kusimamia miamala ya kifedha inayopita kwenye mitandao ya watoa huduma (*mobile money transactions*); ambao umewezesha kupatikana takwimu za huduma za kifedha na kutoa taarifa hizo Benki Kuu ya Tanzania ambaye ni mdhibiti wa huduma za kifedha, na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kama mkusanyaji mkuu wa kodi.

Takwimu za miamala ya fedha zimesaidia kujua kiwango cha fedha kwa njia ya mitandao ya simu na ukuaji wake. Kwa mfano, kiasi cha fedha zilizozungushwa kwenye mitandao ya Kampuni za simu hapa nchini kilikua kutoka wastani wa shilingi trillioni 8.5 kwa mwezi mwaka 2017 hadi wastani wa shilingi trilioni 11.6 kwa mwezi kwa mwaka 2018.

Mfumo huu pia unatupatia takwimu za mauzo ya huduma zote za mawasiliano (sauti, *data*, ujumbe mfupi) na yale ambayo hayana uhusiano na huduma za mawasiliano (*non telecommunications service revenue*) kama vile mauzo ya simu, *modem* na kukodisha eneo.

Mfumo wa TTMS umewezesha kutambua takwimu za mawasiliano ya simu za ndani ya mtandao mmoja (*on-net traffic*) na zile za kutoka katika mtandao mmoja kwenda mtandao mwingine wa mtoa huduma (*off-net traffic*).

Mfumo umewezesha kutambua vyanzo vyote vya mapato ya watoa huduma, pamoja na mapato yote ya mtoa huduma.

Mamlaka ya Mapato Tanzania wamepewa uwezo wa kuingia katika mfumo huu na kupata taarifa za mapato.

TCRA imeendelea kushirikiana na TRA na kufanya mawasiliano ya mara kwa mara juu ya kuboresha na kuimarisha mfumo huu ili kuhakikisha kuwa mfumo huu unawarahisishia majukumu yao ya kukokotoa, kukusanya na kuhakiki kodi stahiki zinazolipwa na kampuni za simu hapa nchini.

Kwa kuzingatia kuwa teknolojia ya mawasiliano inabadilika kila mara, mfumo huu utaendelea kuboreshwa zaidi kwa kuongezewa wigo (*scope*) ili uweze kusimamia mawasiliano yanayotumia *data* kutoa huduma mbadala za simu za sauti na ujumbe mfupi au *over the top technologies (OTT)*, suala ambalo limesababisha mjadala mkubwa kimataifa. Maboresho haya yataongeza pia mapato kwa Serikali.

Aidha, Mfumo unaweza kuongezewa uwezo ili watengenezaji (*manufacturers*) wa vifaa vya mawasiliano ya ki-elektroniki waweze kuchangia gharama za kusimamia na kushughulikia vifaa hivyo vinapomaliza muda wake wa matumizi (*end-of-life management)* hapa nchini. Kwa mfano, utaratibu unaweza kuwekwa kwa watengenezaji wa simu hizi kuchangia gharama za kuchakata taka zinazotokana na vifaa hivi vya kielektroniki pale vinapofikia ukomo wa kutumika. Kwa kuwa mfumo unawezesha kutambua idadi ya simu zote zilizounganishwa pamoja na watengenezaji wa simu hizo, utaratibu wa watengenezaji kuchangia gharama utawezeshwa na takwimu kutoka kwenye Mfumo huu.

Naomba nikuhakikishie kuwa, TCRA itautunza na kuusimamia mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa mawasiliano ya simu (TTMS), kwa maslahi mapana ya Taifa na ustawi wa wananchi wake kwa uadilifu na weledi mkubwa.

Tutahakikisha TTMS inapanuliwa ili kupewa uwezo wa kuhakiki vyanzo vya mapato na mapato yatokanayo na huduma za mawasiliano kadri huduma zitakavyoongezeka.

Pia, TCRA itaendelea kuhakikisha kuwa raslimali adimu (masafa na namba za simu) zinatumika kwa umakini (*efficiently and effectively*) ili kukidhi mahitaji ya Taifa na kuharakisha maendeleo. Tunakushukuru kwa kutuamini kuendelea kulitumikia Taifa hili.

Naomba nihitimishe maelezo ya mfumo kwa kusema kuwa tangu mfumo wa TTMS ulipoanza kufanya kazi, mkandarasi alikuwa anafanya kazi pamoja na watumishi wa TCRA kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuujua na kuuendesha mfumo huo wa TTMS.

Tayari TCRA imefanya mafunzo kwa watumishi wake na wameshaanza kuendesha mfumo huu.

Mafunzo haya ni endelevu ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya TEHAMA yanayotokea hapa nchini na duniani kote.

Baada ya kutoa maelezo juu ya Mfumo wetu wa TTMS naomba niseme machache kuhusu mambo mengine muhimu kwa wadau na watumiaji wa huduma za mawasiliano.

Kufuatia maendeleo na mwingiliano wa kiteknolojia (*technological convergence*), mnamo mwaka 2003, iliyokuwa Tume ya Mawasiliano (TCC) na iliyokuwa Tume ya Utangazaji (TBC) hapa nchini ziliunganishwa na kuanzishwa TCRA.

TCRA ilianzishwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania Na 12 ya 2003 ikiwa na jukumu pana la kusimamia sekta ya mawasiliano nchini Tanzania kwa kutoa leseni kwa makampuni yote ya mawasiliano, ikiwemo ya huduma za simu, utangazaji, intaneti, posta na usafirishaji wa vifurushi.

TCRA inawasimamia watoa huduma za mawasiliano katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inawapa pia raslimali za masafa na namba ili kuwezesha utoaji wa huduma husika na kuhakikisha Sheria, Kanuni na masharti ya leseni vinafuatwa.

Majukumu ya TCRA yameainishwa zaidi kwenye Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Na. 12 ya Mwaka 2003 na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Na. 3 ya Mwaka 2010.

Uwekezaji katika sekta hii ni chachu kubwa ya maendeleo ya uchumi na kijamii kama ilivyo katika uwekezaji wa huduma (*utilities*) nyingine. Mawasiliano bora hupunguza gharama za uzalishaji, kuongeza mapato na kuongeza ajira. Hivyo mawasiliano yana athari za moja kwa moja au zisizo dhahiri (*direct and indirect effects*) katika ukuaji wa uchumi wa viwanda. Mawasiliano yanatoa fursa kubwa kwa wawekezaji kuweza kupata taarifa na mawasiliano yatakayoweza kufanyika kwa maamuzi ya haraka. Pia mawasiliano yanarahisisha mipango ya upatikanaji wa mali ghafi, uzalishaji na masoko.

Sekta ya mawasiliano ni sekta muhimu kiuchumi na ni sekta mtambuka kwa kuwa ni wezeshi ya sekta nyingine katika kuongeza ufanisi wa shughuli mbalimbali za uchumi.

Hapa nchini kwetu, tumeshuhudia ukuaji wa kasi kwa huduma za fedha mtandao ambao umechangiwa sana na kupanuka kwa mitandao ya watoa huduma za simu hapa nchini. Kila palipo na huduma za mawasiliano ya simu, wananchi wanaweza kupata huduma za fedha mtandao.

Aidha upatikanaji wa huduma za fedha-mtandao pamoja na huduma zingine za mawasiliano unahitaji usimamizi mzuri wa raslimali adimu za mawasiliano yaani masafa na namba za simu, jambo ambalo ni moja ya majukumu ya TCRA na hivyo kufanya masafa na namba kuwa vyanzo vikuu vya mapato ya Serikali kupitia TCRA.

TCRA ndio inayopangilia na kutoa masafa na namba fupi; yaani *short codes* zinazotumika katika kufanya miamala ya kifedha kupitia makampuni ya simu.

Kwa kutumia *short codes* zenye mfumo wa *150*(Utambulisho wa Mtoa Huduma)# miamala ya fedha, huduma za benki, michezo ya kubahatisha, uchangishaji wa fedha na huduma nyinginezo nyingi zinapatikana kupitia kwenye simu. Ni dhahiri sasa kwamba kupitia kwenye simu siyo tu ulimwengu wote upo kiganjani bali pia simu imekuwa chombo muhimu na wezeshi katika shughuli za kifedha, kijamii na kiuchumi.

Baadhi ya mafanikio mengine ni pamoja na kuimarishwa kwa usimamizi wa mfumo wa utangazaji wa dijitali ambapo sasa wananchi wanapata taarifa za habari pamoja na habari mbalimbali za kimaendeleo za nchi yetu kutoka kwenye televisheni bila kulipia (FTA) kwa mujibu wa sheria za nchi.

Pia tumeanzisha utaratibu wa usajili wa laini za simu kwa kutumia vitambulisho vya taifa vinavyotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwa kutumia mfumo wa kuchukua alama za vidole (*biometric registration*).

Mfumo huu utachangia kupunguza uhalifu katika mitandao ya simu, usumbufu na mlolongo wa taratibu za kumsajili mteja.

Kanuni za Maudhui Mtandaoni zilizotolewa na Serikali mwezi Machi 2018 zimewezesha kutolewa kwa leseni kwa wamiliki na watoa huduma za maudhui mtandaoni. Kati ya Machi na Disemba 2018, leseni 224 zimetolewa. Kati ya hizi, za blogu ni 93, majukwaa ya majadiliano (*online forums*) mawili (2), redio mtandao 32 na televisheni mtandao 97. Utaratibu wa kutoa leseni za maudhui mtandaoni ni kutambua mchango mzuri wa huduma za maudhui mtandaoni kwa jamii na Taifa lakini pia ni katika kudhibiti matumizi mabaya ya huduma hizo.

TCRA haizuii matumizi ya mitandao ya kijamii au radio na televisheni za mitandaoni bali inalinda maslahi mapana na endelevu ya jamii inayotumia huduma hizo na hasa watoto na jamii kwa ujumla. Milango iko wazi kwa wanaotaka kuanzisha huduma hizi; lakini watatakiwa kuomba leseni.

Katika nyakati hizi na huko tunakoelekea tunashuhudia na tutashuhudia ongezeko kubwa la matumizi ya ama simu au kompyuta na intaneti na si hapa kwetu tu bali ulimwenguni kote.

Tayari tunazungumzia juu ya mifumo ya huduma inayoitwa *Internet of Things* na *Artificial Intelligence* ambayo iko katika hatua mbalimbali katika kila nchi na imeanza kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi duniani. Hivyo masuala ya usalama wa mitandao hayahusu kuwalinda watumiaji tu, bali pia yana umuhimu mkubwa katika kulinda uchumi wa nchi na ulimwengu kwa ujumla hasa ukizingatia kuwa ulimwengu sasa ni kama kijiji kwa jinsi tulivyounganishwa kupitia mawasiliano.

Kwa kuzingatia hili, TCRA inasimamia kituo cha kitaifa (TZ-CERT) kilichoanzishwa mahsusi kwa kulinda mitandao yetu ikiwa ni pamoja na kubaini mashambulizi ya kimtandao (*cyber attacks*). Kupitia kituo hicho, tumeweza kujumuisha na kushirikisha taasisi zenye matumizi makubwa ya kompyuta kama vile vyuo, mabenki na hata taasisi za Serikali kuanzisha vituo vya aina hiyo ili wote kwa pamoja tuweze kushirikiana.

Mpaka sasa tumepata mafanikio makubwa na tutazidi kukiimarisha kituo hiki kimfumo na wataalam wenye ujuzi endelevu ili kwenda sambamba na mabadiliko yanayotokea.

TCRA itaendelea kushirikiana na vyombo na taasisi zingine katika kuboresha usalama mitandaoni na katika kusaidia kuwasaka na kuwanasa wale wote watakaotumia mitandao kwa nia ovu ili wafikishwe katika vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Rais, nitumie fursa hii tena kukushukuru wewe binafsi kwa msukumo wako ulioutoa kuhakikisha kuwa TTMS inakuwa na mfumo wa kuhakiki vyanzo vya mapato yote ya watoa huduma na hivyo kurekebisha mapungufu yaliyokuwepo. Pia napenda niishukuru Kamati iliyoundwa na Katibu Mkuu Kiongozi kwa kufuatilia ukamilikaji wake.

Mwisho naushukuru uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano pamoja na Bodi ya Wakurugenzi ya TCRA ambao walihakikisha utekelezaji wa TTMS unafanyika kwa umakini mkubwa; na kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali na matakwa ya mkataba ili kukidhi matarajio yaliyokusudiwa.

Kwa upande wetu sisi watumishi wote wa TCRA tumetekeleza kwa nguvu zetu zote.

Tanzania Computer Emergency Response Team (TZ-CERT) is a team within the structure of the Tanzania Communication Regulatory Authority (TCRA), with national responsibility for coordinating responses to cyber security incidents at the national level. It cooperates with regional and international entities involved in the management of cyber security incidents. TZ-CERT was established under section 124 of the Electronic and Postal Communications Act (EPOCA) of 2010.

TZ-CERT provides the following services to its constituencies and the general public.

1. Alerts and Warnings

With the growth in cyber threats and vulnerabilities, TZ-CERT constantly monitors cyber security threats and vulnerabilities and advises both its constituencies and the general public.

2. Incidents Response

With expertise in cyber security, TZ-CERT can now work with constituency organizations to respond to all cyber security incidents in their respective networks. TZ-CERT provides step by step assistance to organizations facing cyber security attacks.

3. Cyber Security Awareness

With the mandate of improving cyber security posture in the country, TZ-CERT disseminates cyber security information to the public. This includes promoting cyber security best practices to users of information and communications technologies.

TZ-CERT will work on improving its services and focus on providing other cyber security services to the community including:

- Security audits and assessments
- Malware analysis
- Intrusion detection
- Risk analysis
- Security Consulting.

For more information and to report cyber security incidents please contact TZ-CERT:

Mawasiliano Towers,
20 Sam Nujoma Road
P.O.Box 474,
14414 Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2412 039; +255 22 2199760-9; +255 784558270 – 1.
Fax:+255 22 2412038
Email: info@tzcert.go.tz; incidents@tzcert.go.tz.
PGP Key ID: DFEB96E8
PGP Fingerprint: 38FF 3F79 7E41 8D52 C43C 8C6E 3E53 6C17 DFEB 96E8.

Tanzania Communications Regulatory Authority

ISO 9001:2015 CERTIFIED

Mawasiliano Towers, No. 20 Sam Nujoma, P.O Box 474,
14414 DAR ES SALAAM.
Tel: +255 22 2118947/52;
+255 784 558270
Fax +255 22 2412009 – 10
E-mail: dg@tcra.go.tz
Website: www.tcra.go.tz

ZONAL OFFICES

Lake Zone
NSSF Commercial
Complex,
4th Floor Wing B,
Kenyatta Road,
P. O. Box 3108,
33194 MWANZA.
Tel/Fax: +255 28 250 5081/2
E-mail: mwanza@tcra.go.tz

Northern Zone
Summit Centre, 3rd floor,
Block B
Sokoine Road,
P. O. Box 15675,
23194 ARUSHA
Tel +255 27 254 8947
E-mail: arusha@tcra.go.tz

Zanzibar Office,
19 Mbuyukisutu,
Chukwani Area,
P. O. Box 3284,
71194 ZANZIBAR
Tel/Fax: +255 24 223 5062,
E-mail: zanzibar@tcra.go.tz

Central Zone
LAPF Complex
SIDO AREA
P. O. Box 2229
41194 DODOMA
Tel: + 255 26 232 1731
+255 732 961 625
E-mail: dodoma@tcra.go.tz

**Southern
Highlands Zone**
Century Plaza Building
1st Floor
Tunduma Road,
P. O. Box 1375,
51194 MBEYA.
Tel: +255 25 250 5016,
+255 25 252 5017,
E-mail: mbeya@tcra.
go.tz

Eastern Zone
147 Kajenga Road,
Mikocheni,
P.O Box 35615
14194 Dar Es Salaam
E-mail: easternzone@tcra.
go.tz